

HAIKUWA HIVYO

TANGU MWANZO



Asante, Ndugu Moore.

² Habari za asubuhi, enyi watu. Hakika nilifurahi kuwa hapa asubuhi ya leo tena, wala nisingeukosa huu kwa chochote, kusikia unabii wa dada yetu, kuwa na majaliwa ya kukutana na Ndugu Kidson jana usiku tena, mwenzangu wa zamani, mmoja wa wenzangu wa kwanza katika milki za Kipentekoste. Yeye ndiye aliyenileta hapa Shreveport mara ya kwanza, naamini ndivyo, Ndugu Kidson, miaka mingi iliyopita nilipokuwa na ibada kwenye ile—ile maskani ya kale. Ninaamini huo ndio wakati mamake Ndugu Moore alipoponywa kwenye wakati huo, na, ugonjwa wa tumbo, na mambo mengi aliyofanya Bwana.

³ Unaona, Ujumbe ule ule ungali unaendelea. Hatuyasumbui maagizo hayo, tunayaacha tu jinsi yalivyo, na kuyameza jinsi yalivyopimwa kwetu.

⁴ Ninamthamini ndugu huyu Mwairishi, bila shaka, tuna Mwairishi mzuri, aliyeimba *Kuna Zeri Katika Gileadi*, ulioingiana kikamilifu na jana usiku. Maskini kwaya hii, nzuri, David, na Ndugu na Dada Moore, Anna Jeanne, na hao wote, loo, jamani, ni jambo zuri sana kuwa hapa katika ushirika pamoja nanyi watu tena.

⁵ Nikiwa nimesimama chumbani dakika chache zilizopita, simu ya mbali ilikuja kutoka kwa mtu aliyekuwa mhudumu mahali fulani, ambaye madaktari walikuwa wamemkatia tamaa wala hawakujua alikuwa na shida gani. Akaingia kwenye simu na kupiga, na *kwa njia moja au nyingine*, kupitia ofisini nyumbani, wakampata, walijua tungekuwa maskanini wakati huu, na papo hapo tulipokuwa mle ndani, mimi, Ndugu Kidson, na Ndugu Moore, na ndugu wengine, sikujua ni nani aliyekuwa amesimama pale, bali alitaka kujua matokeo yake yalikuwa nini, mbele za Bwana, iwapo alikuwa anaenda kufa.

⁶ Naye Roho Mtakatifu humo jengoni, ofisini tu dakika chache zilizopita alimfunulia mtu huyo habari zake, na yote kumhusu, na kile alichokuwa, jinsi alivyokuwa amevalia amesimama pale, na shida yake ilikuwa ni nini, na kumtangaza amepona. Nusura aing'oe simu kutoka ilipowekwa, jinsi Bwana alivyomponya.

⁷ Loo, hivi hatuna furaha kwamba tungali tunaye Bwana Mungu, Ambaye angali anaujua mwisho tangu mwanzo? Na ni vizuri kwamba kuna zeri katika Gileadi, na kwa wingi sana, huko kuna madaktari, na chochote kile Bwana alichotuandalia. Kwa hiyo kwa nini tukiendee kitu kingine chochote, wakati

Mungu ametuandalia kwa wingi sana kila furaha tunayohitaji? Na kila baraka tunayohitaji iko katika nyumba ya imani pamoja na watoto wa Mungu.

⁸ Kwa nini turejee, au, tujiepushe na jambo hili, na kuanza kuvuta sigara tupate furaha, kunywa pombe tupate furaha, mambo hayo huleta tu mauti. Hiyo... Furaha yetu ni Bwana. Kwa hiyo nina furaha sana kuwa nikifurahia jambo hilo.

⁹ Sasa, mnaachilia ibada zenu saa ngapi? Saa tano u nusu? [Ndugu Moore anajibu, "Saa saba u nusu."—Mh.] Loo, hilo... Mimi... Msingeweza kunivumilia muda mrefu hivyo. Kwa hiyo nita—nitanini... Nina furaha sana kuona kundi hili hapa nje. Nami sitachukua muda mrefu.

¹⁰ Sasa, usiku wa leo saa kumi na mbili wavulana watakuwa wakigawa kadi za maombi, nasi tutafanya mstari wa kawaida wa maombi. Nitakuwa nikizungumza usiku wa leo, Bwana akipenda, juu ya jambo fulani kuhusu uponyaji wa Kiungu, ama kitu kama hicho, kwa sababu tutaweka wakfu ibada hii usiku wa leo kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu.

¹¹ Mimi na Billy tulikuwa tumeketi mkahawani asubuhi ya leo, tukila, nasi tulikuwa tukiangalia, naye akasema, "Baba, unaweza kuwajua Wakristo wakati unapokutana tu nao, mahali popote?"

Nikasema, "Hakika."

Akasema, "Unamwona yule mtu na mkewe wakiingia mle?" Kasema, "Hao ni Wakristo."

Nikasema, "Naam."

Na katika dakika chache tu mtu mwingine alikuwa ameingia, akasema, "Uh-uh."

Nikasema, "Hiyo ni kweli." Kwa hiyo, katika dakika chache mtu mwingine akaingia, nikasema, "Vipi kuhusu yule?"

Naye akasema, "Hiyo ni kweli."

¹² Daima unaweza kumjua Mkristo, wengi bila shaka ni wanawake wasio na rangi ya makucha, ama chochote ulicho upuuzi huo wanaojipaka, si kujipaka huo, lakini ninamaanisha kwa namna fulani unaweza kuwatambua, unaona, wao—wao wametiwa alama tu. Naye Mkristo ana mazingira, kwa sababu ingawa, yeye ni mwana na binti wa Mungu, yeye ni muumba.

¹³ Maskini jamaa yeyote aliyekuwa akifundisha shule ya Jumapili hapa asubuhi ya leo, hakika ninauthamini ujumbe huo. Alikuwa sawa, niliupenda. Wewe ndiye yule ndugu? Papa *hapa*. Vema, hilo ni sawa. Wewe ulikuwa, hapo awali, hapana shaka ulikuwa Mbaptisti kwa sababu ningeweza kujua jinsi ulivyokuwa ukizungumza, ya kwamba ninyi... Sisi... Kwa namna fulani inaweka alama ndogo huko nyuma, lakini tutaisahau, mnaona. Kwa hiyo... Ndugu zetu Wabaptisti kwa

namna fulani tunaninii tu...mmoja kwa mwingine, lakini ningeweza...

¹⁴ Aliposema, tamshi alilotoa, nililiandika kwenye kipande cha karatasi, nitalichukua huko ofisini, "Wawili wenye nguvu zote walikutana." Hiyo ni kweli. Mungu na mwaminio wanapokutana, hao hapo wawili wenye nguvu zote, maana mtu ni sehemu ya Mungu, yeye ni mwana wa Mungu, mnaona, na kile kidogo alichokinaungana na Mwili mzima. Naye Yesu alisema katika Marko 11:22, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini yale uliyosema, unaweza...yatatimia." Unaona? "Amini yale uliyosema." Naye Mkristo ametiwa alama *sana* hivi kwamba amezungukwa na mazingira.

¹⁵ Je, uliwahi kukutana na watu ambao ulipenda tu kuwa pamoja nao? Umekuwa na hilo, na mbona, wanaunda mazingira hayo kwa maisha ya—yao, jinsi wanavyoishi, na mambo wanayowazia, na upendo walio nao kwako.

¹⁶ Mmesikia ujumbe wangu juu ya yu—yule oposamu, mwajua, na juu ya wale nyuki wakijaribu kuniuama, yule fahali akijaribu kuniua, wanyama, mnaona. I—itifanya...Unaumba mazingira, na hayo ndiyo mazingira unayopaswa kuwamo upate kuwaombea wagonjwa, unaona, ni jambo lile lile. Upendo ndio unaowatoa pepo wachafu.

¹⁷ Sitalitaja hilo jina, ni mmoja tu wa waongofu kwa Bwana niliowaongoza, alikuwa ni kafiri, naye alikuwa akishuka kwenye barabara kuu ya Alcan kwenye msururu wa malori, na—naye akaona jina langu huko juu, ndipo akasema, "Huo ni ulokole." Kwa hiyo, akasimama tu; na ilikuwa huko Canada, huko mbali karibu na Dawson Creek. Usiku huo, kulikuwa na baridi sana ninyi watu wa Louisiana mngefia huko juu, maana nilikuwa karibu kuganda hata nife, nami nina viyoyozi vyote kila mahali sasa, nikijaribu kupata—kupata baridi, hali hii ya joto hapa. Na...Bwana? [Ndugu fulani anamwambia Ndugu Branham jambo fulani—Mh.] Unaipenda, vema.

¹⁸ Kwa hiyo basi tukaingia ndani...akaingia mle ndani, na usiku huo, Wahindi, na kila kitu, kwa hiyo akaona upambanuzi wa Bwana, pasipo kuyajua Maandiko anarudi huko nje na kumpeleka mzee Mhindi juu ya...maskini mtegaji, akamwingiza ndani. Wala tusingeweza kugawa kadi za maombi, kwa hiyo ilimbidi tu kumsukuma jukwaani kadiri alivyoweza, na hatimaye akampeleka huyu mzee Mhindi kule juu. Naye alikuwa akitaka kuninii...Alimjua huyu mzee Mhindi, akasema, "Mtu huyo ana watu wanaomfuata," ye—yeye huzungumza namna hiyo.

¹⁹ Kwa hiyo, akamketisha huyu mzee Mhindi jukwaani. Mara tu alipokuja pale juu, Roho Mtakatifu akamwambia yeye alikuwa ni nani, kasema, "Nawe unaishi mahali fulani, nawe

ni mtegaji. Una watoto watano, watatu wao wavulana na wawili wasichana.” Kasema, “Mmoja wao ameketi kule nyuma, anasomea ukasisi.” Kasema, “Unaugua TB.”

“Kweli.”

²⁰ Kisha kasema, “Mtu aliyekuleta ni maskini jamaa huyu aliyeketi hapa jina lake *Nanii*.” Kasema, “Anashuku.” Hilo lilitosha, akawa mtumishi wa Bwana.

²¹ Si muda mrefu uliopita tulikuwa tukienda pamoja kote nchini, naye akaniambia, akasema, “Ndugu Branham, unajua mke wangu haamini jambo hili,” kisha kasema, “kila usiku ninapoenda kanisani, na kurudi nyumbani,” kasema, “loo, anaanza tu kunipigia kelele mara ninapofika mlangoni,” kisha kasema, “Ninamshika mkono, yeye ni mdogo, na kumshika, nami ninajaribu kumtoa huyo pepo kwa nguvu niwezavyo.” Kasema... Nikumbushe ujumbe wako asubuhi ya leo, bwana. Kasema, “Ninajaribu kumtoa huyo ibilisi, nami nikasema, ‘Ibilisi, toka ndani ya mke wangu! Ibilisi, toka ndani ya mke wangu! Mpenzi, umepagawa na pepo. Toka humo, ewe ibilisi!’”

“Loo,” nikasema, “hilo ni sawa, Ndugu Fandler, lakini u—unaliendea vibaya.”

Naye akasema, “Vema, unaliendeaje?”

²² Nikasema, “Unapokuja nyumbani, mnunulie kifurushi cha peremende, umpe unapoingia mlangoni, mkumbatie.” Nikasema, “Hivyo ndivyo unavyomtoa pepo.”

²³ Upendo huondoa hofu, sivyo? Upendo, marafiki, ulimwengu wote unatamani sana upate upendo. Huo ni mmoja wa mambo makuu tunayoacha nje ya baraka zetu za Kipentekoste, mwingi kupita kiasi, upendo ndio unaoyachanganya pamoja, ndio saruji inayofanya karama na mambo yote ya Mungu kufanya kazi kikamilifu, “Mkipendana ninyi kwa ninyi, hivi watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu.”

Hebu, kabla hatujalikaribia Neno Lake sasa, tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

²⁴ Mwenyezi na Mungu Mwenye nguvu zote, zaidi ya mambo yote tunakushukuru Wewe asubuhi ya leo kwa ajili ya Yesu, Mwanao, na kwa ajili ya upendo Wake kwetu, kwamba wakati tulipokuwa tungali wenye dhambi Yeye alikufa badala yetu, akitupatanisha turudi kwenye ushirika, turudi kwenye uwana kupitia Damu Yake.

²⁵ Nasi tunaomba asubuhi ya leo, ya kwamba kuenezwa kwa Neno kutashika kila moyo, moyo wangu, pia, Bwana. Tuandae kwa ajili ya kuja kwa Bwana kama vile maskini mama huyu alivyotabiri hivi punde ya kwamba tayari ameondoka kwenye Kiti Chake cha Enzi, Yuko njiani. Kweli tunaamini hilo Bwana.

²⁶ Rebeka akimnywesha maji ngamia ambaye angempeleka kumlaki mpenzi wake, hata hivyo hakuwa amewahi kumwona,

bali ilikuwa ni upendo wa kuonana kwa mara ya kwanza. Tunakushukuru Wewe, Bwana. Tunaamini ya kwamba sisi, tutakapomwona, itakuwa ni upendo, tunapojua ya kwamba Yeye Ndiye aliyekufa na kutukomboa.

²⁷ Ndipo katika uwanja huo mkuu mahali fulani kati ya hapa na Utukufuni hapo tutakapomvika taji Mfalme wa mfalme na Bwana wa mabwana, nao Malaika wasimame wameinamisha vichwa wasijue tunalofanya, kamwe hawakupotea kama sisi, na tutakapoimba nyimbo kwamba alitukomboa, ni wakati mtukufu jinsi gani huo utakaokuwa! Tunautazamia wakati huo, mioyo yetu na iandaliwe.

²⁸ Litakase Neno litakalosomwa, na jalia lifanyike Roho na Uzima kwetu, tupate kuyasahihisha maisha yetu, na kumwishia Yeye Yule aliyekufa kwa ajili yetu. Haya tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁹ Fungueni pamoja nami kwa dakika chache tu. Ninataka kusoma Maandiko machache hapa nione kama ninaweza kutoa muktadha fulani Kwake kwa dakika kumi na tano hadi ishirini zijazo. Na, vema, hebu tufungue Mathayo mlango wa 19, tunaposoma:

Ikawa, Yesu alipoyamaliza maneno hayo, akatoka Galilaya, akafika mipaka ya Uyahudi, ng'ambo ya Yordani;

Makutano mengi wakamfuata; akawaponya huko.

Basi Mafarisayo wakamwendea, wakamjaribu, wakimwambia, Je, ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu?

Naye...akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke,

Akasema, Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe: na hao wawili watakuwa mwili mmoja?

Hata wamekuwa si—wamekuwa si wawili tena, bali mmoja... Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe.

Wakamwambia, Jinsi gani basi Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na kumwacha?

Akawaambia, Musa kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu: lakini tangu mwanzo haikuwa hivi.

³⁰ Sasa, ninataka kuchukua mada ndogo asubuhi ya leo, ama—ama, somo, kama tungeliita hivyo, fungu la maneno: *Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo.*

³¹ Sasa, Yesu, wakati alipokuja duniani hapa kufanya ziara Yake ya duniani kwa kusudi la kukomboa kile ambacho Mungu alikuwa amekusudia tangu zamani, Aliwakuta walimu siku hizo wakifundisha mambo ambayo hayakuwa kweli.

³² Sijui kama asingepata baadhi ya mambo yale yale yakiendelea leo kama akija, mambo ambayo hayakuwa kweli. Naye akawaambia . . . Na sababu ya mimi kuchagua somo fulani hili, *Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo*, kwa sababu itatubidi kurudi mwanzoni kuona ukweli wake halisi ni upi. Kila kitu tulicho nacho duniani leo, hakuna chochote kipya, kilianza katika Mwanzo. Mwanzo ndiyo sura ya mbegu.

³³ Kwa hiyo wakati Mungu anapofanya jambo lolote au anapofanya uamuzi, kama ambavyo nimenukuu mara nyingi, kwamba Yeye daima hana budi kudumu na uamuzi Wake. Jinsi hilo linavyopaswa kuangazia imani zetu! Mnaona? Mungu anaposema jambo fulani, Mbingu zote na nchi zitapita, bali hilo haliwezi kupita. Kwa hiyo inapaswa kutupa tabia, inapaswa kutupa imani kuchukua Neno hilo ambalo Yeye amesema, na kwa maisha yetu yote tulishikilie, kwa sababu Yeye hawezi kulibadilisha, ni la *kweli*.

³⁴ Sasa, Mungu hapo mwanzo aliumba vitu vyote, alivifanya katika mfano wa mbegu kwanza, ilikuwa ni mbegu. Ndipo akasema katika Mwanzo 1, “Kila mbegu na iza kwa jinsi yake.” Nami nashangaa tu, kwa kuwa watu sikuote hujaribu kupotosha yale Mungu amefanya, kwa sababu mwanadamu, katika hali yake ya kuanguka, anafikiri kwamba anaweza kufanya jambo bora zaidi kuliko Muumba wake alivyolifanya hapo mwanzo, yeye daima anajaribu kugeuza kitu ambacho Mungu alifanya na kukifanya kitu ambacho sicho.

³⁵ Nilikuwa nikizungumza juu ya hilo hivi majuzi tu juu ya mahubiri ya *Dini Chotara*. Nayo sayansi, katika kufanya kazi katika uwanja wa sayansi, wale wanaodai mageuzi yanayoendelea wamechukua mathibitisho yao wenyewe ya kisayansi, na, au, thibitisho na kukanusha nadharia yao wenyewe ya mageuzi yanayoendelea, kwa sababu chochote kilicho chotara hakiwezi kujizaa tena. Kwa hiyo kama Yeye aliumba mbegu fulani haina budi kubaki hivyo, kama ukiichanganya na kitu kingine, haiwezi kujizaa tena, hiyo inaimaliza mara tu u—unapoizalisha.

³⁶ Nyumbu, nyumbu kamwe hawezi kumzaa nyumbu mwingine. Kamwe mtu yeyote asimsingizie Mungu kumfanya nyumbu, Yeye hakulifanya, hilo lilifanywa na mwanadamu. Ni—ni ninii. . . Inanikumbusha, ukiwa mwerevu leo, kwa maumbile, unapozalisha chochote kichotara, unaharibu asili yake.

³⁷ Unapomchukua farasi ambaye ni mzuri, farasi ukoo safi, farasi huyo ana tabia yake, ni mpole, utakiinua kichwa chake, nawe unaweza kumwita, ataweka kichwa chake juu ya mabega

yako na kulialia, na—nawe unaweza kumfanya, kumweka kwenye maonyesho, naye ataninii, karibu kama mwanadamu. Anaweza... Ana tabia nzuri sana, na kitu fulani kumhusu ambacho ni halisi. Hujawahi kumwona nyumbu akifanya hivyo, yeye ni—yeye ni mnyama mchapa kazi tu. Yeye ni—yeye ni matendo tu bila neema.

³⁸ Inanikumbusha juu ya watu wengi sana siku hizi. Wewe... Wote ni matendo tu, na ni hayo tu. Kama vile Ndugu Jack alivyokuwa akisema asubuhi ya leo kuhusu makanisa, ya kwamba yana muundo lakini si ninii... Ni kama ninii, una injini nzuri lakini haina mvuke ndani yake, una dainamo, bali haifanyi kazi, jambo kuu ni ule mvuke kwenye injini. Huo ndio kanisa linahitaji, lina jengo.

³⁹ Hebu mchukue nyumbu, yeye—yeye ni—yeye ndiye kitu kijinga kuliko vyote ulimwenguni, kwa sababu yeye ni chotara. Nawe unaweza kumwita nyumbu, naye atasimama tu hapo na kuinua hayo masikio makubwa na kukuangalia.

⁴⁰ Mwajua, na—natumaini hili halisikiki la kukufuru, lakini inanikumbusha juu ya watu wengi sana siku hizi walio na dini ya nyumbu, dini chotara. “Kanisa letu, tunajua yote kulihusu.” Nawe unaweza kuwaambia kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuwapa kanuni za Mungu, nao wanasimama tu huku wameyainua masikio yao, kamwe hawasogei. Chotara mzuri huleta... Ni...

⁴¹ “Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu,” wanajua yaliyo kweli kwa sababu wanapenda Chakula cha kondoo.

⁴² Mbegu chotara kama mahindi, mnaona, inaonekana nzuri, kwa sababu ni chotara. Nilionga kwenye ubao hivi majuzi, “Mahindi chotara.” Vema, hayafai kitu. Unajua inachofanya? Ng’ombe chotara hufanya ng’ombe bora. Kuku chotara, wana kuku walio chotara sana sasa, hata hao kuku hawana miguu wala mabawa, wote ni kifua, bali maskini kitu hicho kinaweza tu kuishi mwaka mmoja halafu kinakufa, karibu amekufa anapozaliwa.

⁴³ Kwa hiyo, watu hawana budi kumla huyo, na sasa kwenye seli hizo ni chotara, sayansi, *Reader’s Digest* iliandika makala juu yake, hivi majuzi, kwamba katika miaka ishirini tangu sasa kama hilo likiendelea, jamii ya binadamu itakwisha. Wanawake na wanaume wanapotoshwa. Wanawake wanakuwa na mabega mapana na nyonga nyembamba, wanaume wanakuwa na mabega membamba na nyonga pana zaidi, mwanamke hataweza kumzaa mtoto wake, akila seli ambayo imepotoshwa.

⁴⁴ Kuku, na kuku hawa mnaowala ni—ni rojorojo sana na laini, umbile asili ndani yao, mpaka watu hawawataki tena. Mbona, mnaninii, wanajiua kwa mawazo yao wenyewe, wakijaribu kupotosha. Tuliumbwa tupate kula seli hizi za—za vitu jinsi tu Mungu alivyoziweka.

45 Na pia kuna kanisa chotara, ni la kupendeza zaidi siku hizi kuliko lilivyokuwa, lina wafuasi bora zaidi, kanisa la Kipentekoste, wana majengo mazuri zaidi, viti bora zaidi, wahubiri waliofunzwa vizuri zaidi, na kadhalika, bali wamelichanganya.

46 Hebu turudi kwenye ile Nuru halisi, ya kwanza, ile baraka ya kale ya Kipentekoste, na nguvu za Roho Mtakatifu zirudi kanisani. Wameweka yote juu ya mhubiri siku hizi. Si mhubiri, Roho Mtakatifu ni mwingi tu kwa walei kadiri alivyo kwa mhubiri. Yeye hana dini yote, wanayo *huko* nje. Na mimi—mimi ni mmoja leo anayeamini ya kwamba tunapaswa kumrudisha Roho wa Mungu kanisani, ambapo tunaweza kuwa na karama za Roho zikitenda kazi kwa upako na nguvu.

47 Lakini leo tunaona watu ambapo, hapo mwanzo (Katika *Nyakati za Kanisa* ninazofundisha juma lijalo kwenye maskani yangu nyumbani, kuandika maelezo madogo kama maoni yangu mwenyewe juu yake.), mnaona, matendo ya Wanikolai yalianza, baada ya kitambo kidogo yakawa fundisho. Vema, jambo ni kwamba, waliondoa Roho wote kutoka kwenye kusanyiko, wakafanya maaskofu, waangalizi, mapapa, wakamweka wote mimbarani, ndipo mimbara ikawa ni ya kiakili, hapo mna kanisa chotara tena, mnaona, chini ya wasomi.

48 Mungu uturudishe kwa Roho Mtakatifu miongoni mwa watu. jalia upako wa Roho utende kazi miongoni mwa watu, ukitoa jumbe, na nguvu, na madhihirisho, ikitubidi kusimama pembeni mwa barabara, ama kuingia kwenye banda la kuku, ama kibanda mahali fulani.

49 Hatutaki yoyote ya dini hii chotara inayotoka kwenye seminari, tunamtaka, aje kama upepo wa nguvu ukienda kasi kutoka Juu unaoijaza nyumba yote, si mtu mmoja tu, nyumba yote ambamo wameketi pamoja. Upotovu, hivyo ndivyo mwanadamu alivyofanya katika siku za Bwana wetu Yesu, hivyo ndivyo anavyojaribu kufanya leo, kuchukua vitu ambavyo ni vya asili, na kupipotosha kwa mawazo yake mwenyewe, naye anajiingamiza mwenyewe.

50 Ningependa kumwuliza mwanamageuzi yaendeleayo hivi: Kama huwezi kuzalisha tena mahindi chotara, wanawezaje kamwe kufundisha mageuzi yanayoendelea? Mungu alisema, “Kila mbegu na izea kwa jinsi yake,” kila mbegu kwa jinsi yake. Na kama ukiichanganya mbegu hiyo, imekwisha, haiwezi kwenda mbali zaidi, inarudi moja kwa moja kwenye asili yake tena.

51 Nina furaha sana kwamba ninaamini ya kwamba Mungu alipanda Mbegu ya Roho Mtakatifu kwenye Siku ya Pentekoste, wameichanganya ikawa madhehebu, lakini baada ya kitambo kidogo itarudi kwenye asili Yake tena, irudi kwenye Roho Mtakatifu halisi, irudi kwenye Ujumbe wa Injili, irudi kwenye

Matendo 2 tena, irudi kwenye ile fomula, irudi mahali ilipoanzia. Atainuka mtu moja ya siku hizi ambaye atapinga mambo haya, na kuyashambulia kwa nguvu awezavyo.

⁵² Angalieni sasa, kwenye ile ya asili, rudini kwenye mwanzo, Yesu aliwaambia, “Rudini kwenye mwanzo mpate kujua. Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

Vema, watu wanasema, “Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni *hiki*. Mimi ni *kile*.”

⁵³ Hilo ni sawa, lakini hebu turudi kwenye mwanzo, tuone mahali ilipoanzia, tuone ilivyokuwa hapo mwanzo. Hivyo ni, jinsi Mungu alivyoliweka Kanisa Lake kwenye Siku ya Pentekoste, hivyo ndivyo, linapaswa kudumu hivyo milele. Kama ukilichanganya na chochote kile, madhehebu, na mambo haya mengine yote, na kunyunyizia, na taratibu hizi zote na kadhalika, unalifanya chotara. Utapata kanisa linaloonekana bora zaidi, bali halina Uzima ndani yake, haliwezi kujizaa tena.

⁵⁴ Ule uamsho uliotokea katika siku za Luther, hauwezi kujizaa tena, kwa sababu waliufanya chotara; siku za Wesley, hawawezi kuzaa tena. Niambie moja la hayo lililopata kuinuka lilipoanguka. Wanapolifanya kanisa chotara, linarudi nyuma moja kwa moja tena, limekwisha, haliwezi kujizaa tena, linaweza kuwaingiza washiriki, liunde dhehebu, bali haliwezi kujizaa tena. Tunachotaka ni *kitu* cha kuzaa tena, kuwaleta wana na binti kwa Mungu. Huwezi kufanya hivyo kutoka kwenye seminari, haina budi kuja kutoka kwa Roho Mtakatifu juu, kama upepo wa nguvu ukienda kasi, kama ulivyofanya hapo mwanzo.

⁵⁵ Dini chotara zikipotosha mambo, zikibadilisha mambo, watu wikipotoka. Ndipo Yesu alipokuja katika siku Zake, alisema, “Mnaniabudu bure, mkifundisha Mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.” Wamefanya nini? Walizichukua amri za Mungu na kuzichanganya na mawazo yao wenyewe, na wameyarudisha, na kusema, “Usininii, nawe utafanya *hivi*,” na kadhalika, bali wao kwa mapokeo yao huzitangua amri za Mungu, kwa sababu walikuwa wamezichanganya.

⁵⁶ Watu wanashangaa siku hizi jinsi mambo haya yanavyotukia. Mtu anawezaje kusimama, na kuangalia kwenye kusanyiko, na kumvuta mwanamume ama mwanamke, na kuzifunua dhambi, na kadhalika, za kanisa? Kuna nini? Mbona ninii, makanisa yote hayafanyi hivyo? Wao ni chotara. Hiyo ni kweli.

⁵⁷ Kuna Kanisa moja tu, nalo si dhehebu, huwezi kuliundia dhehebu Kanisa la Mungu. Kuna Kanisa moja na Mwili mmoja, Mwili huo ni Mwili wa kisiri wa Yesu Kristo hapa duniani, “Na kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili huo mmoja,” kama sisi ni Wamethodisti, Wabaptisti, ama Wakatoliki, ama chochote kile.

⁵⁸ Haidhuru dhehebu la mtu ni lipi, kama analitegemea kanisa lake kwa ajili ya wokovu, amepotea. Kama Mkatoliki anategemea kanisa Katoliki kumwoko, amepotea; kama Mbaptisti anategemea kanisa la Kibaptisti kumwoko, amepotea; kama Mpentekoste anategemea kanisa la Kipentekoste kumwoko, amepotea, lakini kama hao watu binafsi wanategemea Mungu na Yesu Kristo, “Kwa imani mmeokolewa, na hiyo si kwa matendo, bali kwa neema.”

⁵⁹ Yesu aliwakuta walimu katika siku Zake, pia, wakipotosha mambo, naye akawaambia ya kwamba hapo—hapo mwanzo. . . Tunaona jambo lile lile leo, wanasema, “Loo, naam, Biblia kweli inasema Yesu Kristo ni yeye yule jana na hata milele, *bali* hatuamini Yeye angali anafanya miujiza. Tunaamini ya kwamba Yesu alisema, ‘Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya,’ *bali* tu—tunaamini ya kwamba mambo hayo yalikoma na mitume.”

⁶⁰ Unaona kile unachofanya? Unalichanganya, unalipotosha, ukisema jambo ambalo Mungu hakusema. Biblia inasema, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Ninaamini *hilo* kuwa ni kweli. Siamini tunapaswa kuvuruga hilo hata kidogo, tuseme tu lipo, kama huna imani ya kuendelea nalo, usimzuie mtu mwingine ambaye ana imani ya kuendelea.

⁶¹ Sikuzote nimesema, “Laiti ningalikuwa na imani ya kutembea, kama Henoko, kwenda Nyumbani pamoja na Mungu, bila mauti, lakini kama sina imani ya namna hiyo, hakika sitaki kumzuia mtu ambaye ana imani hiyo ya kutembea. Nitamwacha aendele mbele.” Hakika, nami nitaomba ya kwamba Mungu atanipa neema na nguvu za kusonga mbele. Hakika.

⁶² Yesu alilikuta kanisa, wakati alipokuja, likilitumainia kanisa kwa ajili ya wokovu. Hilo ni jambo lile lile a—analofanya siku hizi, wakati amekuja katika umbo la Roho Mtakatifu katika siku hizi za mwisho, Anawakuta watu wakilitumainia kanisa kwa ajili ya wokovu. Watu walipata nini katika siku za Yesu walipokuja, wakitumainia kanisa kwa ajili ya wokovu? Walipata lundo la kanuni za imani, mafundisho ya sharti ya kujibunia, wakilipotosha Neno la Mungu kulirudisha kwenye kanuni ya imani.

⁶³ Hilo ndilo jambo lile lile tulilo nalo siku hizi. Wakati Roho Mtakatifu akiwa hapa, ule Utu wa Roho Mtakatifu, akisaka, akimtafuta Bibi-arusi wa Kristo, tunapata nini? Anakuta nini? Watu wakikubali kanuni za imani kwa ajili ya wokovu, badala ya kurudi kwenye ya asili kwa ajili yake. Mna ki—kitabu cha maombi, ama namna fulani ya kitabu cha kiada cha namna fulani ambacho, “Sisi *Fulani-na-fulani* tunaamini *hivi-na-hivi*.”

⁶⁴ Kwa nini uchukue kitabu cha kiada kwa ajili yake? Biblia ya Mungu ndiyo Kitabu cha kiada, rudini kwenye mwanzo. Mnachukua kupeana mikono, badala ya ubatizo; mnachukua

kunyunyiziwa, badala ya ubatizo wa maji; mnachukua taratibu na kanuni za imani, na kadhalika, badala ya kuchukua ile fomula jinsi Mungu alivyoandika, hiyo ndiyo sababu tuna kanisa chotara, lililokufa siku hizi, kwa sababu haliwezi kuzaa tena. Mlutheri anaweza kufanya Mlutheri, Mbaptisti anaweza kufanya Mbaptisti, Mpresbiteri anaweza kufanya Mpresbiteri, bali Mungu humfanya mtakatifu Yeye anapoingia ndani, Roho Mtakatifu wa asili, baraka za Kipentekoste.

⁶⁵ Walikuwa wakitarajia kanisa liwape wokovu, ndipo wanakuta kwamba hata hawakujua Shina lenyewe la wokovu wao wakati Yeye alipokuja, kwa sababu walikuwa chotara. Walimwambia kama kundi la nyumbu, “Huh, u nani wewe? Ulizaliwa mwana haramu.” Kama maskini punda anayelialia mahali fulani, mwajua, huko nje, “Siku za miujiza zimepita. Musa alifanya *hivi-na-vile*, lakini jamaa huyu ni nani? Yeye si wa lolote la madhehebu yetu. Aa, ni telepathia, hivyo tu. Yeye ni Beelzebuli, ibilisi.”

⁶⁶ Jambo lilo hilo limetukia tena. Hawamjui Kristo katika nguvu za kufufuka Kwake; wanamjua kwa kanuni ya imani bali si katika nguvu za kufufuka Kwake. Kristo anaishi ndani ya huyo mtu, na kama angekuja leo, na tuwasikie watu wakisema mambo wanayofanya, Yesu kwa urahisi angesema tu, “Haikuwa hivyo tangu mwanzo.”

“Mbona,” angesema, “Bwana, nilinyunyiziwa katika kanisa takatifu *Fulani-fulani*.”

Angesema, “Haikuwa hivyo tangu mwanzo.”

“Vema, nilipeana mikono na mhubiri, na kukiri.”

“Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

⁶⁷ Walingojea hapo mwanzo hata nguvu zilipokuja kutoka Juu, Upepo Wenye nguvu Unaoenda kasi uliobadilisha mwelekeo wote wa maisha yao, na kuwatia moto kwa Kitu fulani kilichouinjilisha ulimwengu.

⁶⁸ Tunawezaje kufanya hivyo kupitia kusoma, kuandika, na hisabati? Yesu alisema, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili.” Sio, “Kufundisha kusoma, kuandika na hisabati.” “Kuhubiri Injili” Injili ni nini? Injili ni nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu. Fuatilia Maneno yanayofuata, “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

⁶⁹ Utamfundishaje mtu kunena kwa lugha? Utamfundishaje mtu kutoa pepo kwa nguvu? Utamfundishaje mtu kufanya ishara hizi ambazo Yesu alisema angefanya? Utamfundishaje mtu kuweza kusimama jukwaani, na, ama mahali fulani, na kutabiri mambo yajayo, na mambo ambayo yamekuwako, na yatakayokuwako? Utamfundishaje? Huwezi, ni karama ya Mungu. Tunapoliondokea jambo hilo, tunaingia katika hali ya uhotara. Tumerudi, tunarudi tu kwenye mwanzo, kila mbege.

⁷⁰ Sijui, ningetaka sayansi ijibu hili: Kama kuna kitu kama mageuzi yanayoendelea, nao wanadai yangeweza kuja kwa njia nyingine, kwa nini kitu fulani kisiinuke juu kuliko mwanadamu? Hatuna spishi iliyo juu kuliko mwanadamu. Kwa kuwa yeye yuko katika sura ya Mungu, hakuna kitu kinachoweza kupita Muumba wake. Ningependa wao walijibu hilo. Hawawezi kulijibu. Kwa nini? Ndiyo spishi iliyo juu zaidi.

⁷¹ Kwa nini hatuwezi kutoa kitu fulani katika maadili yetu, na elimu, na seminari zetu kuu kitakachoshinda kile walichokuwa nacho kwenye Pentekoste. Huwezi kufanya hivyo, kwa sababu hiyo ni njia ya Mungu ya kulifanya. Hakuna kitu kitakachotokea ambacho kita—kitaichangamsha mioyo ya watu, kitakachotoa ishara hizi. Kamwe hutawaelimisha watu waingie ndani yake, kamwe hutaweza kuwafundisha watu waingie ndani yake, hawana budi kuzaliwa ndani yake. Kwa hiyo madhehebu yetu ni chotara.

⁷² Tunahitaji Roho Mtakatifu, Mwili wa kisiri wa Kristo ukiumbika duniani. Hivyo ndivyo ilivyokuwa hapo mwanzo, linajizalisha tena na kurudi moja kwa moja kwenye mwanzo. Katika miaka hii yote ya madhehebu, hatimaye, Mungu amelirudisha Kanisa Lake kwa Roho Mtakatifu tena. Nina furaha sana kuwa ndani Yake. Acha mbegu za kale na mambo ya kimwili yafe, niwe kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Tumeketi pamoja leo katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu.

⁷³ Roho Mtakatifu akizaa, loo, nina furaha sana kwa jambo hilo, akiyaondoa mashaka, akiziondolea mbali itikadi, akijizalia ndani Yake wana wa Mungu. Sio kuwazaa tena nyumbu, kuwachanganyisha, bali kuwazaa wana na binti za Mungu ambao hawaangalii Neno, na kuinua masikio yao na kusema, “Vema, mama yangu alikuwa Mpresbiteri.”

⁷⁴ Hiyo ni sawa, bali tunahitaji kwanza kujifanya wana na binti za Mungu, tukiondolea mbali kutokuamini, na kanuni za imani, na kadhalika na kuturudisha kwa wana wa asili wa Mungu kwa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli kabisa. Hivyo ndivyo Kanisa linavyoendelea kufanya leo.

⁷⁵ Basi watu siku hizi wako kama wale wa kale, wanalichotarisha kanisa kwa dhehebu, kwa kanuni za imani, na kuzichanganyisha akili za watu, na halafu wanasema, “Yuko wapi Mungu? Yuko wapi Mungu wa Agano la Kale? Yuko wapi Bwana Yesu aliyeahidi mambo haya?”

⁷⁶ Hilo ndilo Billy Graham alilokabiliwa nalo si muda mrefu uliopita, mnaona, na Mwislamu, “Yu wapi Mungu huyu unayenena habari zake? Yeye alisema aliwaponya wagonjwa. Nitawachukua thelathini, nawe uwachukue thelathini, tuone kile tunachoweza kufanya juu yake.”

⁷⁷ Loo, tunachohitaji leo ni mtu hodari, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, kumpa changamoto. Hiyo ni kweli. Mungu angali ni

Mungu aliyekuwa pamoja na Eliya kwenye Mlima Karmeli, Yeye angali ni Mungu yeye yule leo. Tunahitaji dini iliyozalishwa na Roho Mtakatifu, nguvu za Roho Mtakatifu.

⁷⁸ Mungu yuko wapi? Mungu yuko katika Kanisa Lake, Mungu yuko katika Neno Lake, Mungu yuko ndani ya watu Wake, Mungu yuko katika ulimwengu Wake, Yuko kila mahali. Ila hatuwezi kumchanganya katika kitu fulani, kwa sababu hatachanganyika na chochote, Yeye ni Mungu na Mungu pekee. Huwezi kumzalisha katika vitu vitano ama sita mbalimbali, na—na Miungu wanne ama watano mbalimbali, Yeye ni Mungu na Mungu peke yake, hatachanganya mbegu, Yeye ni Mungu.

⁷⁹ Huwezi kufanya maombezi ya watakatifu, na kusema, “Mtakatifu *huyu* alifanya *hivi*, na mtakatifu *yule* alifanya *vile*.”

⁸⁰ Hakuna kitu kama hicho. “Kuna Mpatanishi mmoja kati ya Mungu na mwanadamu, na huyo ni Kristo Yesu,” Mpatanishi pekee.

⁸¹ Kanisa lina shida gani basi? Kama Yeye angekuwa hapa duniani, ambapo Yuko, nasi tunaona kanisa siku hizi katika hali ile ile Yeye aliyoliona, likifundisha Mafundisho yaliyo maagizo ya mwanadamu, Yeye alisema, “Haikuwa hivyo tangu mwanzo.” Sasa tunaona jinsi ilivyokuwa hapo mwanzo.

⁸² Inanikumbusha siku moja wakati, Yusufu na Mariamu walipokuwa wamepanda kwenda kwenye karamu, nao walikuwa wameanza safari yao wakirudi, nao walikuwa wameenda safari ya siku tatu, nao wakamkosa Bwana Yesu, hawakujua alipokuwa. Sasa, siku tatu bila kujua alikuwa wapi. Ndipo tunaona kwamba walianza kumtafuta. Kanisa limeenda karibu miaka elfu mbili wala halijui mahali Yeye alipo. Wakizungumza kuhusu siku zao tatu!

“Loo,” walisema tu, “labda, Yeye yuko miongoni mwa jamaa zetu huko nje, mahali fulani.”

⁸³ Hivyo ndivyo kanisa limekuwa likiwazia, “Loo, Yeye yuko huku, mahali fulani, kama hayuko pamoja nasi Wabaptisti, atakuwa pamoja na Wamethodisti, na Yeye, loo, Yeye yuko huku, mahali fulani. Yuko pamoja na baadhi ya jamaa zetu. Mwajua, huko nyuma kabisa babu zetu—zetu Wamethodisti walikuwa, na babu zetu Walutheri . . .”

⁸⁴ Usilichukulie vii hivi tu namna hiyo, hebu tumtafute. Yuko wapi Mungu wa Biblia? Yuko wapi Mungu aliyetoa ahadi hizi? Yeye ni nani? Jina Lake ni nani? Kwa nini hatuwezi kufanya mambo yale yale waliyofanya huko nyuma kama waliyaahidi? Kwa nini ni vivyo hivyo?

⁸⁵ Si muda mrefu uliopita nilikuwa nikiwinda kuchakulo. Niliilenga bunduki yangu kwenye yadi hamsini. Kama siwezi kulipiga risasi jicho la huyo kuchakulo, ninaachana naye. Endapo niko yadi thelathini kutoka kwake, nitarudi nyuma

zifike hamsini, nihakikishe nimempata. Ndipo bunduki yangu ikaenda kombo, nami nikairudisha kwa Kampuni ya Winchester, bunduki ndogo, ya bei rahisi, wakanijibu, kasema, “Kasisi Branham, bunduki hii ita—itaenda kombo inchi moja kwenye yadi ishirini na tano. Katika Winchester Muundo 75, hayo tu ndiyo utakayopata kwake.”

⁸⁶ Nilijua vizuri zaidi ya hayo, nimekuwa huko chini kwenye safu rasmi ya yadi hamsini, nikaitumia kulenga misumari minane ya zulia, moja kwa moja, nami nilijua hawakuwa sahihi. Mnaona? Nami huyo hapo, nilikuwa nimefanya kila kitu, nikalegeza skrubu, na kuzikaza kwa sababu ya mtetemo wa tano kwa elfu moja *hapa* utaitupa kando inchi moja huko nje kwenye yadi hamsini. Nami nilikuwa nimeikaza, na kuhakikisha haigusi mtutu, na kufanya yote niliyojua kufanya.

⁸⁷ Nami ni—nilijua bunduki ile ile, Gene Goad aliyeketi hapa, rafiki yangu, anajua hivi majuzi nililenga misumari minane, tisa, risasi tisa kwenye shimo lile lile, umbali huo. Lakini kampuni iliyoitengeneza ilisema kitu hicho—kitu hicho kitakosa shabaha, hiyo ni kukosa shabaha, mwajua, ya risasi, yapata inchi moja kwenye yadi ishirini na tano, nayo hii ilikuwa ikipiga shabaha kwenye yadi hamsini.

⁸⁸ Nilikuwa nimeketi chini ya mti, na kulikuwako na Ndugu Wood na hao wengine huko juu wakiwapiga risasi kuchakulo, wanampiga popote walipotaka, nyuma, mbele, popote, haikuleta tofauti yoyote, maadamu walimpiga huyo kuchakulo, wakiwa na wakati mzuri. Nami nilikuwa nimeketi chini ya mti, nikaanza kulia, kisha nikasema, “Bwana, kwa nini ukanifanya maskini mnyonge na mwenye wasiwasi hivi. Mbona ukaniumba hivi? Kwa nini siwezi kwenda huko nje na kufurahia kuwinda kama wanavyofanya, na inilazimu kuiweka bunduki hii katika hali kamilifu sana?”

⁸⁹ Nikangojea pale kwa karibu nusu saa, na kujilaza kifudifudi, nikaanza kulia, Roho Mtakatifu akanijia, na kusema, “Nilikuumba namna hiyo kwa kusudi fulani, hilo ni kwa kusudi fulani. Mtu anaposema jambo *moja*, na kulenga ovyo namna hiyo, huwezi kulivumilia isipokuwa inalenga kikamilifu, haina budi kuwa kwenye alama, la sivyo si sahihi.”

Nikasema, “Naona, Bwana.” Mnaona?

⁹⁰ Madhehebu tu ya kanisa hayaniridhishi. Kama Maandiko yanasema jambo *moja*, nalo kanisa linafundisha *lingine*, hilo halifai kitu. Kama Yesu Kristo aliishi ndani ya mitume, na kufanya ishara alizofanya alipokuwa hapa duniani, zitajirudia kama tutalenga kikamilifu. Hatuna budi kulenga kikamilifu! Sijali kanisa linasema nini, itakosa shabaha *hivi* na *vile*, na, “Loo, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, na upuuzi wa namna hii nyingine yote, na kanuni hizi zote za imani, na kadhalika; njia *moja* ama *nyingine* ni sawa.”

91 Si sawa kwangu. Kama mitume walipiga ile alama, tunaweza kupiga hiyo alama, pia, kama tutalenga kikamilifu kwa Neno la Mungu. Hebu ujuzi wetu ulenge kwa na Neno Lake, walifanya hivyo. Kama walifanya hivyo, kwa nini sisi tusifanye hivyo? Kama tutalenga kikamilifu, litafanya jambo lile lile.

92 Loo, kanisa linasema, “Maadamu inapiga, maadamu unajiunga na kanisa unapeana mikono na mchungaji, na kuandika jina lako kwenye kitabu, na kukariri kanuni hii ya imani, imani hii ya mitume, basi inaleta tofauti gani?”

Inaleta tofauti kubwa sana, Roho Mtakatifu anakuelekeza kimamilifu kwenye Neno la Mungu.

93 Yesu, walimtarajia kuwa pamoja na jamaa Zake; hivyo ndivyo tumetarajia, “Loo, Yeye alikuwa pamoja—Yeye alikuwa pamoja na Martin Luther, alikuwa pamoja na John Wesley, John Smith, Calvin, Alexander Campbell, ama baadhi yao, Yeye alikuwa pamoja nao.”

Hilo halitafaa kitu. Hivi Yeye yuko pamoja nasi?

94 Kwa hiyo, wakaanza kuangalia pande zote siku moja. Mnajua mahali walipompata? Si pamoja na jamaa zao, si pamoja na mashirika yao, si pamoja na madhehebu yao, pamoja na wale waliomtarajia kuwa nao.

95 Hivyo ndivyo tumekuwa tukifanya, tumekuwa tukijaribu kuwa na uamsho. Billy Graham amevuka nchi, Jack Shuler, loo, wengine wengi walijaribu kufanya uamsho. Wanafanya na nini? Juu ya mambo ya kiakili, kuwaleta Wabaptisti wote pamoja, Wamethodisti wote pamoja, Wapresbiteri pamoja, kuwaweka pamoja, kuyaleta hayo mashirika, kufanya viongozi, kuwazungumzia na kuwachochea, na kadhalika namna hiyo, kupeana mikono, kuwa sawa. Hilo—hilo ni zuri.

Kama yule mtu mweusi, akila tikitimaji, alikula kipande chake. Kasema, “Ilikuwa je, jamani?”

Kasema, “Hiyo ilikuwa ni tamu, naomba *nyingine*.”

96 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, kukusanyika pamoja na kupeana mikono ni sawa, bali kuna mengine zaidi. Amina. Kuna zaidi ya hayo. Haidhuru ni wasomi wangapi tutakaokusanya pamoja, jinsi tunavyofanya, ule Uhai haupo, hatuna budi kurudi mahali tulipomwacha Kristo.

97 Martha, ama, Mariamu na—na Yusufu walirudi mahali walipomwacha. Walimwacha wapi? Kwenye Sikukuu ya Pentekoste, si kwenye kanisa la Kilutheri, si kwenye kanisa la Kimethodisti, si kwenye ule msingi huko—huko Uingereza, si Calvin, Knox, Finney, hao watu walikuwa wazuri, kamwe hatukumwacha mwanzoni mwa madhehebu yetu, tulimwacha kwenye Sikukuu ya Pentekoste. Hapo ndipo kanisa halina budi kurudi tena, hapo ndipo mtakapompata, si kanisani mwenu, si

katika dhehebu lenu, si pamoja na dini ya mama yako, dini ya baba yako, utampata kwenye Karamu ya Pentekoste.

⁹⁸ *Brrrrr!* Najua mnafikiri mimi nina kichaa. Labda ninatenda hivyo, lakini ninajisikia tofauti. Angalia, ndugu, rudini kwenye Pentekoste. Tumeenda mbali sana sasa, tumeichukua Pentekoste na kuiundia madhehebu, na kuiundia madhehebu, na kuiundia madhehebu, na kuiundia madhehebu, tukaunda dhehebu *hili*, tukagombania *hili*, *lile*, na *linginelo*. Kushikana mikono ni sawa, hilo halitoshi, hebu na turudi kwenye ya asili, turudi kwenye mwanzo, turudi mahali tulipoliachia. Amina. Nisikieni! Ninanena katika Jina la Bwana: Rudini kwenye mwanzo.

“Unasema mimi ni Mmethodisti.”

“Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

“Nilinyunyiziwa.”

“Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

“Mimi ni Mbaptisti.”

“Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

“Mimi ni Mpresbiteri.”

“Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

⁹⁹ Hapo mwanzo, ilikuwa ni Pentekoste, si dhehebu, bali tukio la Kipentekoste lililoishusha Mbegu ya Mungu kwa Roho Mtakatifu, ikawafanya wanaume na wanawake kunena kwa lugha na kuyumbayumba kama watu walevi, Roho akitenda kazi Kanisani, akionyesha ishara na maajabu.

“Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

Unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa lile kanisa kuu, takatifu.”

“Hiyo haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

“Mimi ni wa Warumi watakatifu. Mimi . . .”

“Haikuwa hivyo hapo mwanzo.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁰⁰ Kama kamwe likichipusha tawi lingine, litakuwa ni tawi la Kipentekoste. Litakuwa na matunda yale yale, ishara zile zile, maajabu yale yale ambayo tawi la kwanza lilitoa.

Unasema, “Mimi ni Mlutheri.”

¹⁰¹ “Haikuwa hivyo hapo mwanzo.” Umepandikizwa na unaishi kwa Jina la Bwana Yesu wakati huzai tunda hilo. Ishara za waaminio hazikufuati.

¹⁰² “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Nao wakaenda wakihubiri kila mahali, Bwana akitenda kazi pamoja nao, akilithibitisha Neno kwa ishara zilizofuatana nao.” Tukiwa na chochote tofauti na hilo, “Haikuwa hivyo hapo mwanzo.” Jinsi

walivyompokea Roho Mtakatifu hapo mwanzo, hivyo ndivyo tunavyompokea leo.

Unasema, “Vema, si—sijui, nina, ninaamini, labda, wakati nilipoamini nilimpokea Roho Mtakatifu.”

“Haikuwa hivyo hapo mwanzo.” Waliamini, *halafu* wakampokea Roho Mtakatifu.

¹⁰³ Paulo alisema katika Matendo 19 kwa hao Wabaptisti kule juu waliokuwa na yule mwanasheria mhubiri aliyeongoka, Apolo, alisema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?”

Unaposema ulimpokea ulipoamini, basi, “Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

Unasema, “Nimenyunyiziwa, nami nasema . . .”

“Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

“Nilijiunga . . .”

“Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

¹⁰⁴ Kamwe hawakujiunga na kanisa lolote hapo mwanzo, *walizaliwa* Kanisani hapo mwanzo. Na kama hiyo . . . Hiyo ni kweli, unazaliwa ndani Yake. Na kama Mzabibu huu ukipata kuchipusha tawi lingine, litakuwa ninii, kama tawi . . . Kama huo Mzabibu ukiwahi kuzaa tawi lingine, litakuwa ni tawi la aina ile ile ambalo Matendo iliandikwa juu yake. Litakuwa na Fundisho lile lile, litakuwa na nguvu zile zile, litaonyesha ishara zile zile, kwa sababu hilo ndilo Kanisa walilokuwa nalo hapo mwanzo.

¹⁰⁵ Hebu tuache kujifanya chotara, hebu turudi kwenye Neno, kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Mnapenda hilo? Ninaishi kwa hilo.

Hebu na tuzungumze Naye sasa aliyeandika hayo, tunapoinamisha vichwa vyetu.

¹⁰⁶ Kuna yeyote humu ndani asubuhi ya leo anayejisikia kana kwamba umechanganyikiwa mahali fulani, nawe ungetaka Roho Mtakatifu aingie asubuhi ya leo, kwa kuzaliwa?

¹⁰⁷ Basi uchotara ulikuwa ni jambo baya sana katika Agano la Kale, Yeye alisema, “Mtoto haramu hataingia katika kusanyiko la Bwana kwa vizazi kumi.” Hakuna kitu cha kumwondolea, ila dhambi hiyo tu. Wazieni, vizazi kumi, miaka mia nne kabla mtoto haramu hajaweza kuingia katika Ufalme wa Mungu. Hakukuwako na seramu ya kumhudumia nayo, ilimbidi tu kuiondoa kupitia kwa jamaa. Miaka mia nne kabla ya mtoto haramu kuingia katika kusanyiko la Bwana.

¹⁰⁸ Lakini siku hizi, kwa kuwa Damu ya Yesu Kristo imemwagwa, nanyi mmechanganyishwa na mawazo ya kila namna, Roho Mtakatifu yuko hapa asubuhi ya leo kuwazalisha kuwarudisha kwenye ule wa asili, kuwarudisha kwenye

Pentekoste, kuwazaa tena. Nasi tumeketi pamoja asubuhi ya leo katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tukimruhusu Roho Mtakatifu... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...?... *Kutahiri* ni nini? Kukatilia mbali uhotara wote, mambo ya ziada, mambo ya ulimwengu, mambo ya wakati wa kanisa, akiturudisha kwenye Pentekoste, kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

¹⁰⁹ Je, ungependa kupokea tukio hili, na ungetaka maombi kwamba ungempokea, na kurudi mwanzoni na kuwa na Uzima wenyewe wa Kristo ukiishi ndani yako, ukitoa ishara alizofanya Yeye alipokuwa hapa duniani? Mwaweza kuinua mikono yenu kwa ajili ya maombi, kabla tu hatujaomba? Mungu awabariki. Mungu awabariki, mikono tu kila mahali.

¹¹⁰ Bwana mwenye rehema, tunakushukuru asubuhi ya leo kwa ajili ya Neno Lako. Ni kali, ni la kweli, bali ni U—Upanga. Nao upanga uliorekebisha hunolewa. Nao una nguvu, Ni Mtambuzi wa mawazo ya, makusudi ya moyo. Tunakushukuru asubuhi ya leo kwa ajili ya Neno Lako, ingawa linakata, hutahiri. Hiyo ndiyo sababu ni Upanga, ni wa kututahiri kutoka kwa mambo yote ya ulimwengu, na kutuingiza katika ushirika pamoja na Wewe kama wana na binti za Mungu tukiketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu.

¹¹¹ Mungu alituchagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu ili tuwe watakatifu na wasio na hatia mbele Zake, tukiishi katika utakatifu katika mazingira ya usafi, tukikiri kwamba sisi ni wasafiri katika dunia hii. Tu wageni, sisi si wa hapa, urithi wetu ni wa huko Juu. Tunaotazamia Mji huo ujao, ambao Mjenzi na Mwenye kuubuni ni Mungu. Tunasikia kutoka kwake kila siku na kila saa, huku baraka za Roho Mtakatifu zikimiminika juu yetu tunapoketi pamoja tukifundisha na kukusifu Wewe.

¹¹² Tunaomba sasa kwa ajili ya mikono hii iliyoinuliwa. Mungu, hii ndiyo saa ya uaminifu, ni wakati ambapo watu, wakiitazama dunia, na hofu juu yao kwa ajili ya mambo yajayo. Hawataki kitu tu ambacho ni cha bandia, wanataka kitu imara, wanataka kitu ambacho ni halisi. Na Baba, wanapoyaona maisha yao, ambamo wamepandikizwa, hawazai matunda, ishara za Mzabibu wa kwanza hazimo ndani yao, wameinua mikono yao, “Bwana, ondoa *hili*, na unijalie nipitie kwenye Tawi la kweli.”

¹¹³ Mungu, ninaomba asubuhi ya leo ya kwamba Roho Mtakatifu atawazaa tena, awazae tena kutoka kwa mashaka yao yote kwamba Yesu huponya, yale mashaka ya kwamba Roho Mtakatifu ni kuisimkwa tu kwa ulokole, nao, kama watu wasemavyo ndivyo alivyo, kisha jalia mashaka yote yaondoke, na kujua ni Bwana Yesu aliyebarikiwa mbele zetu, Yeye anajithibitisha Mwenyewe.

¹¹⁴ Pia yafungue macho ya watu, usiwaache waishi kama walivyoishi katika siku za—za mitume, katika siku za manabii. Hakuna nabii aliyejulikana sana na mtu yeyote, mpaka baada ya kifo chake. Yesu hakujulikana, wengi wa watakatifu kabla ya hao hawakujulikana kamwe, Ujumbe hupita, nao wanaukosa. Kanisa hili litanyakuliwa moja ya siku hizi na kutwaliwa, ndipo watapiga mayowe, “Nipe Mafuta,” lakini hakuna mengine ya kununuliwa wakati huo. Jalia wasiyakose asubuhi ya leo, Bwana, bali kwa unyenyekevu, jalia wakutafute Wewe kwa moyo wao wote.

¹¹⁵ Sasa Baba, siwezi kukuleta Wewe kwao, wala hao Kwako, ninaweza tu kunena yale Wewe umesema na mpango uliosema Wewe, “Yeye atakayeyasikia Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele.” Ninaomba, Mungu, ya kwamba kila mtu humu ndani asiye na Roho Mtakatifu aweze kurudi kwenye mwanzo asubuhi ya leo. Sio, haiwabidi kuliacha kanisa lao, warudi tu kwenye mwanzo, na kupandikizwa, ama, sio kupandikizwa, bali kuzaliwa mle ndani. Mzabibu hiliopandikizwa ni kwa dhehebu, kamwe hautasimama. Ninaomba ya kwamba watazaliwa katika Roho, katika Mzabibu, kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

¹¹⁶ Ninawakabidhi Kwako, Baba. Ninaomba ya kwamba utawabariki kupitia siku hii. Tusaidie, yatakase mawazo na mioyo yetu. Na usiku wa leo, wakati mkutano wa maombi ukiendelea kwa ajili ya wagonjwa, jalia kuwe na nguvu zisizoneneka miongoni mwetu, jalia kuwe na mioyo iliyotakaswa na Roho Mtakatifu, mashaka yote na fadhaa zote zimeondoka. Yesu Kristo yu hai, Naye yuko pamoja nasi sasa. Tujalie, Bwana.

¹¹⁷ Bariiki kanisa hili, mbariki Ndugu Jack, Dada Moore, na—na Anna Jeanne, na Don, na wote wanaoshiriki hapa, Ndugu Lyle, Ndugu Brown, na wengi sana wao, Baba, nisingeweza kuwataja, kila mhudumu, Ndugu Kidson, wahudumu wengine wote hapa, Ndugu Bootlayer, na wengi ambao—ambao hata hatuwajui.

¹¹⁸ Bwana, ziwasho moto nafsi zetu. Mungu, jalia turudi, upesi. Tunazungumza juu yake, lakini mazungumzo hayatafanya kazi, hebu turudi nyuma. “Yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi.” Ni kutokuamini, dhambi ni kutokuamini. Hatuliamini kama tukilisema wala haturudi. Hebu turudi kwenye mwanzo. Uchukue Ujumbe, Bwana, na kuutupilia nje kwa watu. Tunaona Roho Mtakatifu akitenda kazi tena, kama alivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste. Sikia maombi yangu kwa ajili yao, Baba, katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

¹¹⁹ Mungu awabariki. Na, mchungaji wenu. 

60-1127M Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo
Life Tabernacle
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org